



CHRISTIAN SOCIAL SERVICES COMMISSION

An Ecumenical Body of Tanzania Episcopal Conference and Christian Council of Tanzania

P.O. Box 9433, Dar es Salaam, Tanzania

CSSC - MTHANI WA PAMOJA KIDATO CHA PILI, NYANDA ZA JUU KUSINI 2026

MWONGOZO WA UTAHINI

1.

i.	ii.	iii.	iv.	v.	vi.	vii.	viii.	ix.	x.
D	B	C	A	D	A	C	A	A	D

Alama 01 @ = alama 10

2.

i.	ii.	iii.	iv.	v.
F	B	D	I	H

Alama 01 @ = alama 05

3. Mafunzo katika kujenga tabia njema yalisisitiza mambo yafuatayo:-

- ✓ Utunzaji wa wazee, watoto na wasiojiweza.
- ✓ Uwajibikaji na kufanya kazi kwa bidi
- ✓ Ukakamavu, uhodari na ujasiri
- ✓ Kuheshimu wazee na watu wakubwa kiumri
- ✓ Kushirikiana katika mambo yote ya furaha na huzuni kama vile harusi na misiba,
- ✓ Kuisitiza kupenda na kukarimu wageni.
- ✓ Kujenga uhusiano mwema katika jamii, hivyo malumbano ya moja kwa moja yalikesewa.

Alama 02 @ = alama 10

4. Sababu za jamii za Kitanzania kupinga ulipaji wa kodi ulioanzishwa na utawala wa Kijerumani

- ✓ Kodi ilikuwa njia ya kuwakandamiza na kuwanyima uhuru Watanzani
- ✓ Jamii za kitanzania hazikuona manufaa ya moja kwa moja ya ulipaji wa kodi kwa ajili ya ustawi wa jamii zao
- ✓ Jamii zilipinga ulipaji wa kodi kama njia ya kulinda uhuru wao
- ✓ Kodi ilipingwa kwa sababu ulikuwa ni utamaduni mpya kwa jamii za kitanzania
- ✓ Kodi ilipingwa kwa sababu ilitakiwa ilipwe kwa fedha tasilimu, utaratibu ambao hawakuwa wameuzoea.

Alama 02 @ = alama 10

5. Kutoa maana za maneno yafuatayo kama zinavyotumika katika somo la historia ya Tanzania na maadili

- Tanganyika Territory Civil Servants' Association (TTCSA)**, ni chama cha wafanyakazi kilichoanzishwa na Mrtin Kayamba mwaka 1922 huko

Tanga, ambacho 1924 kilifungua tawi lake Dar es Salaam. Chama hiki kilitoa mchango wake mkubwa katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika.

ii. **All Muslim National Union of Tanganyika (AMNUT)**, ni chama cha kisiasa kilichoundwa mwaka 1959. Kiliundwa kwa ajili ya kupambania uhuru wa Tanganyika. Chama hiki kilidai uhuru lakini kilitaka mabadiliko ya katiba na uhuru viletwe polepole na si haraka kama TANU ilivyotaka.

iii. **Tume ya Rais ya Kudumu ya Uchunguzi ya mwaka 1966**, (*The Presidential Permanent Commission of Enquiry*) ilikuwa ni tume iliyoundwa kuchunguza mwenendo wa viongozi na watumishi wa umma waliokuwa wakikiuka maadili, kujilimbikizia mali na kutumia madaraka vibaya kinyume na miiko ya chama cha TANU, ambacho mara kwa mara ilikemea vitendo vya rushwa. Tume ya Rais ya Kudumu ya Uchunguzi ya mwaka 1966, llichangia Kamati Kuu ya TANU kutangaza Azimio la Arusha mwaka 1967, lililoweka miiko mbalimbali yenye misingi ya utu na usawa katika jamii, mambo ambayo yalisaidia katika mapambano dhidi ya rushwa.

iv. Vyama vya ushirika, ni muunganiko wa watu waliokubaliana kuendesha shughuri zao za kiuchumi kwa pamoja ili kuinua hali zao za maisha. Watu hawa walitakiwa kuwa na mahitaji yanayofanana ya kupata huduma ya shughuli yoyote ya kiuchumi iliyowafanya waanzishe chama. Mfano wa vyama hivi ni **Bukoba Buhaya Union (1924) chini ya Clemence Kiiza na Rwamugira na Kilimanjaro Native Planters Association (1925) chini ya Joseph Merinyo**

v. Jando na unyago, ni sherehe za kimila ambazo hutolewa kwa vijana, jando kwa upande wa kiume hufanywa wakati wa tohara na huambatana na mafunzo kwa vijana wa kiume. Unyago kwa upande wa vijana wakike kuwaweka tayari kwa ajili ya kukabiliana na majukumu katika jamii.

Alama 02 @ = alama 10

6. Sababu zilizofanya Waingereza kubadilisha mfumo wa utawala kutoka utawala wa moja kwa moja hadi mfumo wa utawala wa kiwakala

- ✓ Hawakuwa na nguvu kazi ya kutosha
- ✓ Kupunguza gharama za kuendesha utawala
- ✓ Kuwepo kwa miundombinu duni ya usafirishaji na mawasiliano
- ✓ Kikwazo cha lugha baina yao na jamii za kitanzania
- ✓ Kuzuia uinzani kutoka kwa jamii za kitanzania
- ✓ Kuhakikisha wananyonya maliasili za Tanzania kiurahisi Zaidi

Alama 02 @ = alama 10

7. Faida za maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia katika kuyadumisha mavazi ya asili.

- ✓ imesaidia katika uboreshaji wa nguo
- ✓ imesaidia mavazi kudumu kwa muda mrefu
- ✓ imerahisisha upatikanaji wa masoko kutoka na bidhaa hii kuzalishwa kwa ubora
- ✓ imesaidia kuongezeka kwa ubunifu
- ✓ uzalishaji wa mavazi umeongezeka mara dufu *Alama 02 @ = alama 10*

8. Nafasi na mchango mkubwa wa vijana katika kukuza na kuenzi maadili ya taifa hili kwa manufaa ya taifa la leo na la kesho
- ✓ Kutoa elimu na uhamasishaji kuhusu maadili
 - ✓ Vijana kuwa mifano ya kuigwa na wanajamii
 - ✓ Kutumia mitandao ya kijamii kwa maudhui chanya
 - ✓ Uanzishaji wa vikundi vya kijamii kukuza maadili
 - ✓ Kushiriki katika shughuli za kijamii kama ndoa, matambiko nk
 - ✓ Kushiriki katika shughuli za uongozi katika jamii
 - ✓ Kushiriki katika shughuli za Sanaa na utamaduni kueneza maadili
- Alama 02 @ = alama 10*
9. Madai ya vyama vya wafanyakazi kipindi cha harakati za kudai uhuru

Hivi ni vyama vilivyoanzishwa na waafrika waliokuwa wameajiriwa katika viwanda, mashamba, bandari na sehemu nyingine kwa lengo la kudai na kutetea masilahi yao ya kikazi. Madai yao yalikuwa kama yafuatayo

- ✓ Kudai kulipwa mishahara kwa wakati
- ✓ Kuongezewa msharaha kulingana na kazi
- ✓ Kuwekewa mazingira bora ya kazi
- ✓ Kupinga ubaguzi kazini
- ✓ Kupinga unyanyasaji kazini
- ✓ Kupunguza muda au masaa ya kazi
- ✓ Kupinga kodi za kinyonyaji *Alama 02 @ = alama 10*

10. Umuhimu wa sera ya Afrikanaizesheni mara baada ya uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar?

Sera ya Afrikanaizesheni

Hii ni sera iliyowapa madaraka Watanganyika na Wazanzibar wazawa. Sera hii ililenga kutoa nafasi za uongozi na ajira kwa wazawa amabazo awali zilishikiliwa na wazungu na Waasia katika utawala wa kikoloni. Watanganyika na wazanzibari wenye ujuzi walihamasishwa kufanya kazi serikalini na katika mashirika ya umma.

- ✓ Ilisaidia kuimarisha udhibiti wa uchumi na siasa baada ya uhuru
- ✓ Ilichangia Kuimarisha uzalendo na umoja wa kitaifa
- ✓ Ilisaidia Kuboresha uchumi wa wazawa
- ✓ Ilijenga utamaduni na utambulisho wa kiafrika

- ✓ Ilisaidia kuondoa Kuondoa athari za ukoloni
- ✓ Kulinda maadili, utu na heshima ya jamii za Tanzania

Utangulizi alama 1.5

Kiini, alama 02 @ hoja = alama 12

Hitimisho alama 1.5

Jumla alama 15